REVIVAL NEWS
From Revival Ministries Australia
P.O. Box 2718 BC TOOWOOMBA Q4350 Australia
Phone: 61-7-46130633; e-mail: rma@revivalministries.org.au
Website: www.revivalministries.org.au

****** JULAI 2020 **** JULAI 2020 **** JULAI 2020 **** JULAI 2020 ******

SEMA NENO TU!

Bibilia ni nini?

"Kila andiko,lenye pumzi ya Mungu,lafaa kwa mafundisho,na kwa kuwaonya watu makossa yao,na kuwaongoza,na kwa kuwaadhibisha katika haki ili mtu wa mungu awe kamili,amekamilishwa apate kutenda kila jambo jema"2 Tim.3:16-17.
Kila andika linarejelea vitabu vya andiko ambavyo tumevipokea,yaani vitabu 39 vya Agano la kale na vitabu 27 vya Agano Jipya.Bibilia ni vitabu vya andiko ambavyo tumevipokea.

Sema neno tu! Hubiri na kufundisha kile kilichoandikwa. Kuna njaa ya neno safi la Mungu katika kanisa duniani kote.

Nani aliandika Bibilia?

Petro anarejelea Andiko kama neno la kinabii. "Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi,ambalo mkiliangalia,kama taa ing'aayo mahali penye giza,mwafanya vyema ,mpaka kutakapopambazuka,na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu. Mkijua neno hili kwanza,ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu ;bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu,wakiongozwa na Roho Mtakatifu" 1Petro 1:19-21.Watu watakatifu waliandika walivyoongozwa au kubebwa na Roho Mtakatifu.
Hawa watu watakatifu hawakuandika ufasiri wao wenyewe wa kile Roho alinena bali waliandika kama Roho alivyowasukuma.

Walimu waongo

Mpaka siku ya leo shida kubwa kabisa katika kanisa duniani kote ufasiri wa neno la Mungu ambao watu hufundisha na kuhubiri. Walimu huja na mafundisho ya msingi katika Maandiko lakini hawafundishi Maandiko hasa. Petro alituonya,"kutakuwa na walimu wa uongo miongoni mwenu,watakaoingiza kwa werevu uzushi wa kupoteza,wakimkana hata Bwana aliyewanunua,wakijiletea uharibifu usiokawia"(2Pet.2:1).

Hawa walimu na wahubiri wa uongo kwa jumla wana tabia ya matarajio na hata kudai malipo ya pesa kwa unenaji wao. "Na katika kutamani watajipatia faida kwenu kwa maneno yaliyotungwa"(2Pet.2:3a).

Katika mahali pengi ambapo tumekuwa katika miaka ya hivi majuzi na hasa katika mataifa ya Amerika Kusini,tumekutana na mwamko wa mitume na walimu wa uongo, wahubiri wakidai pesa na kutowakilisha huduma ya sehemu tano vizuri. Hii imezaa tunda baya na kuchanganyikiwa na viongozi wengi wa kweli wamenyamazia kupokea mafundisho ya kitume kwa sababu ya matukio yaliopita.

Tunafaa kuzingatia onyo la Isaya, “Na waende kwa sharia na ushuhuda;ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili,bila shaka kwa hao hapana asubuhi”8:20.

Usiende kupita kile kilichoandikwa

Katika waraka wa kwanza kwa Wakorintho,Paulo anawaonya waumini dhidi ya kufuata kiongozi fulani wa kitume-“Maana hapo mtu mmoja asemapo,Mimi ni wa Paulo;na mwingine,Mimi ni wa Apolo,au Mimi ni wa Kefa”(1Kor.1:12).Paulo anaonyesha kazi tofauti ambazo kila mhudumu anayo: “Mimi nilipanda,Apolo akatia maji,bali mwenye kukuza ni Mungu”.(1Kor.3:6).

Kila mhudumu lazima ahukumiwe na neno ambalo limeandikwa: “Basi ndugu,mambo hayo nimeyafanya kuwa mfano wa mimi na Apolo kwa ajili yenu,ili kwamba kwa mfano wetu mpate kujifunza kutopita yale yaliyoandikwa;ili mmoja wenu asijivune kwa ajili ya huyu,kinyume cha mwenziwe”1 Kor.4:6.

NENO HUFANYA KAZI

Tayari tumejifunza kutoka kwa 2 Timotheo 3:16 kwamba Maandiko yanafaa kwa mafundisho,kuwaonya watu makosa yao,kuwaongoza na kuwaadhibisha katika haki”.Kwa kufundisha na kuhubiri neno la Mungu kama vile limeandikwa tunashuhudia neno likifanya kazi. Wasikilizaji wanasadikishwa;wasikilizaji wanapokea hekima na ufunuo kwa Roho(Waefeso 1:17);Roho huleta ufahamu kwa mioyo ya wasikilizaji(Waefeso 1:18).

Hatufai kuongeza kwa Andiko,wala kutoa kutoka kwalo.

Hatufai kutumia Maandiko kuhalalisha fundisho lisilo la Kimaandiko,
Hatufai kuchukua Maandiko na kuyatumia nje ya muktadha,
Hatufai kufanya Maandiko kusema kitu hata kinyume cha yale ambayo yanasema kwenye muktadha .

Katika Waebrania milango ya 3-4,mwandishi anaongea kuhusu kumtambua Yesu aliye Kristo kama Mtume na Kuhani Mkuu(3:1) na kuhusu sisi kujengwa kuwa nyumba yake(3:3-6).Kisha anasawazisha hii na kuingia raha ya Mungu. Tunafaa kuwa watiifu kwa Yesu kama Mtume na Kuhani Mkuu na kujengwa sawasawa kwa nyumba yake,kanisa. Mwandishi anaendelea kuongea kwa nguvu kuhusu kuingia rahani,kuhusu kusikia sauti yake,kuhusu kutofanya mioyo yetu kuwa mzito(3:7-19).

Tukiamini neno la Mungu,tunaingia rahani.
Kisha mwandishi anatupa ufunguo wa kuingia raha ya Mungu:
“Maana neno la Mungu li hai,tena lina nguvu,tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili,tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho,na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya mioyo” Waebrania 4:12.Katika msitari huu neno linatumika kwa roho ya mwanadamu,kubainisha roho kutoka kwa nafsi;neno linatumika kwa nafsi ya mwanadamu,kupambanua fikra na nia ya moyo;na neno linatumika kwa mwili ya asili,hata kuleta uponyaji kwa sehemu za siri za mwili.

Neno la Mungu ndilo kitu pekee katika ulimwengu ambalo linaweza kupenya na kubainisha kati ya nafsi na roho ya mwanadamu. Fikra za kidini na filosofia katika kivuli cha dini za dunia,kujumuisha dini ya kienyeji ya kikristo,zinajua tu binadamu kama kiumbe cha sehemu mbili,yaani,zinazojumuisha ‘nafsi’,inayorejelea sehemu isiyoonekana ya binadamu,na mwili,ikiwa ni binadamu anayeonekana.

Wakati mwingine huo mgawanyiko unarejelewa kama nia na maumbile au eneo la kiroho na eneo la kiasili. Lakini ni kupitia kwa neno la Mungu kufanya kazi ndani yetu tunaposikia na kupokea neno litokalo juu,lakini limeandikwa kwenye Andiko,,ambapo tunasukumwa na kubadilishwa,hata kugeuzwa!

Katika muktadha wa Waebrania 3-4,kuingia raha ni kuja kwa kiti cha enzi cha neema kwa imani katika neno la Mungu,na kupokea neno kwa furaha ili liweze kutubadilisha .Kisha tunaweza kupokea rehema na neema wakati wa mahitaji(4:16).

Imeandikwa

Yesu alipokutana na majaribu katika Mathayo 4 na Luka 4,alimshinda shetani kwa kujua yale yaliyoandikwa kwenye Maandiko na kuweza kuyaleta hayo Maandiko katika mawazo wakati wa hatari. Shetani alimjaribu Yesu kwa kunukuu Maandiko vibaya. Yesu alimshinda shetani wazi kwa kunukuu yale yaliyoandikwa.

Huu uwezo wa kunena neno katika wakati wa changamoto,wakati wa hatari ni kazi ya Roho Mtakatifu na ni dhihirisho ya neno la “rhema”.Neno la “rhema” kubainishwa na neno la “logos” ni neno ambalo limehuishwa kwa ufahamu wetu na Roho Mtakatifu. Yesu hasa alisema, “Mtu hataishi kwa mkate tu,ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu”(Mat.4:4).

Ufunuo ni nini?

Kwa kujibu swali la Yesu katika Mathayo 16:16, Petro alisema, “Wewe ndiwe Kristo,Mwana wa Mungu aliye hai”. Yesu alijibu na kumwambia, “Heri wewe Simoni Bar-yona;kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili,bali Baba yangu aliye mbinguni”(mst.17).Ufunuo huo ulimjia Petro kutoka kwa Baba aliye mbinguni,lakini neno ambalo Petro alitumia kwa Yesu liliandikwa katika Maandiko ya Agano la Kale. Petro yaweza kuwa alifundishwa haya Maandiko na kama wayahudi wengine wengi,alikuwa anatarajia Masiha kuja.Ufunuo ambao Petro alipokea ulikuwa kujua kwamba Yesu ndiye.
Hakuna ufunuo nje ya yale yaliyoandikwa . Mtu akikujia akisema ‘ufunuo’ na hauonekani wazi katika Maandiko ,basi ufunuo huo hautoki kwa Mungu. Ufunuo ni wa uguzo wa kimbinguni kwa neno la Mungu lililoandikwa.

Kuendelea katika neno

Yesu alisema , “Mkikaa katika neno langu [logos],mmekuwa wanafunzi wangu kweli,kweli;tena mtaifahamu kweli,nayo hiyo kweli itawaweka huru”(Yn.8:31-32).Yesu alisema , “Neno lako ni kweli”(Yn.17:17).Yesu anasawazisha kweli na neno la Baba,ambalo ni neno lililoandikwa, ambao ni Maandiko Matakatifu. Kwa hivyo,wanafunzi wanafaa kuendelea katika neno,kufundishwa jinsi ya kufahamu neno,jinsi ya kusoma neno,na jinsi ya kushiriki neno na wengine.

Kuomba kulingana na neno

Yesu alisema, “Ninyi mkikaa ndani yangu,na maneno yangu yakikaa ndani yenu,ombeni mtakalo lote nanyi mtapewa”(Yn.15:7).Hili ndilo neno la ‘rhema’ katika msitari huu,lakini neno la ‘rhema’ silo tofauti na neno la logos;ni neno la logos lililohuishwa.
Kwa hivyo,kama wanafunzi wa neno la logos,maombi yetu yanayoonyesha neno(logos) ambalo limehuishwa kwetu(rhema), yatajibiwa.Maombi kama haya yako katika mapenzi kamili ya Mungu kwa vile ni tunda la neno la Mungu kuwa ndani yetu.

YESU NDIYE NENO

“Hapo mwanzo kulikuwako Neno [Logos],naye Neno alikuwako kwa Mungu ,naye Neno alikuwa Mungu”Yn.1:1.
Neno au mawasiliano ya Mungu yalikuwa na Mungu hapo mwanzo na alikuwa Mungu. Mungu na neno lake hawatenganishwi;hii siyo rejeleo kwa watu wawili bali ina ufunuo wa ndani wa yule Mungu ni nani,na kwa hivyo twamjua Yesu ni nani. Kwa hakika msitari huu unasema, “na Mungu alikuwa Neno”..Katika maandishi ya kiasili kuna msemo wa wazi kwamba Mungu ndiye Neno! Wao ni mmoja na ni sawa.

Mungu hujidhihirisha kupitia neno lake.

Mungu hajulikani kwa njia nyingine yo yote. Yesu ndiye Neno;Neno ni Mungu;na Neno la Mungu limeandikwa kwetu ili tuweze kumjua Mungu kupitia kwa neno lake.
Hakuna chanzo kingine ambako tunaweza kibinafsi kumjua Mungu aishiye milele ambaye aliviumba vitu vyote.Mamlaka yetu tu kwa imani na matendo ni neno la Mungu,ambalo limeandikwa.Wahubiri na walimu wanapofundisha kuhusu Mungu kwa lugha ya teolojia ambayo si ya Maandiko kiwazi, basi lazima tukosoe mafundisho yao. Ujuzi wa Mungu hauna msingi kwa akili au maelekezo yetu [haijalishi tuna shahada ngapi], lakini ujuzi wa Mungu una msingi katika yale yaliyoandikwa katika neno lake.

Ni wakati wa kurudi kwa neno

Tunafaa kuhubiri na kufundisha yaliyoandikwa kwa uaminifu,hiyo inamaanisha kwamba tufundishe na kuhubiri kwa uaminifu Yesu aliye Kristo(Mat.5:42).Vyuo vya Bibilia na seminari hufundisha mafundishi mbalimbali,teolojia,eskatolojia,historia ya kanisa na vitu vingine,lakini Yesu alifundisha neno na kutuma mitume kufundisha neno. Kanisa la kwanza lilijitoa kwa mafundisho ya mitume,hayo yalikuwa mafundisho ya Kristo.Ni wakati wa sisi sote kurudi kwa Bibilia,lile lililoandikwa.
Kama vile mtu alivyosema wakati mmoja: Hapo mwanzo kulikuwa neno,sio tafsiri!

Mfano wa kutoa msitari nje ya muktadha

Mfano wa kutoa msitari nje ya muktadha na kuufanya kusema kinyume kabisa kile kinachosema katika muktadha ni Matayo 24:40. Inasema, “Wakati ule watu wawili watakuwako kondeni; mmoja atwaliwa, mmoja aachwa”.Katika muktadha huo Yesu anarejelea kuja kwake kwa mtajo wa siku za Nuhu, “Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu” (mst.37). Anaongea juu ya wasioamini katika siku ya Nuhu “wakila na kunywa, wakioa na kuolewa ,hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina wasitambue, hata gharika ikaja,ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake mwana wa Adamu”(mst.38-39).

Nani alichukuliwa na gharika? Jibu:wale ambao hawakuamini na walikataa kuingia kwenye safina.Walichukuliwa na gharika.Yesu alisema kwamba kuja kwa Mwana wa Adamu kutakuwa hivyo.

Kwa hivyo,nani anachukuliwa? Nani anaachwa nyuma? Katika muktadha huo ni wazi kabisa kwamba waovu wanachukuliwa na hukumu; kwamba wenye haki wanahifadhiwa katika dunia kupitia wokovu. Na ilhali kanisani kote duniani, imefundishwa kwamba Mathayo 24:40 inarejelea unyakuzi wa wenye haki. Huu ni mfano wa kuchukua Andiko nje ya muktadha na kulifanya kusema kinyume kabisa na maana yake ilivyoandikwa kwenye Maandiko.

Paul Galligan.